**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA KWAHANI

Dodoma, 02 Mei, 2024

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akimtaarifu Mwenyekiti wa Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi ya ubunge katika Jimbo la Kwahani lililopo Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Spika ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka, 2024.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 49(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Kwahani lililopo Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Ratiba ya uchaguzi mdogo utakaofanyika ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Tukio | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. | Fomu za uteuzi | Tarehe 17/05/2024 hadi 23/05/2024 |
| 2. | Uteuzi wa wagombea | Tarehe 23/05/2024 |
| 3. | Kampeni za uchaguzi | Tarehe 24/05/2024 hadi 07/06/2024 |
| 4. | Siku ya uchaguzi | Tarehe 08/06/2024 |

Tume inatumia nafasi hii kuvikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi cha uchaguzi huu mdogo.

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

Scanned with AnyScanner